

USHAHIDI WA ROHO MTAKATIFU

Yohana 14:26 Lakini huyo msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyo waambia.

Mjumbe wa wakati huu anasema yafuatayo:

Leo nilikuwa nikizungumza na rafiki yangu mwema, basi aliniuliza wakati mmoja vile nilivyofikiria juu ya ushahidi wa kwanza wa Roho Mtakatifu, “ULIKUWA ni kunena kwa Lugha?” (Ndio imekuwa miaka mingi iliyopita.) “Nikasema” wala mimi silioni hivyo. “Akasema” hata mimi silioni hivyo, “Ingawa nimefundishwa hivyo Akasema unafikiri ushahidi wake ni nini?

Nikasema, “Ushahidi kamili kabisa ninaoweza kufikiria ni, Upendo.” Na kwa hiyo tukaingilia kuzungumzia jambo hilo. Na kwa hiyo ni kawaza ya kwamba hilo lilionekana zuri sana. Kwa hiyo nikashikilia hilo tu, “kama mtu ana Upendo.” Bali siku moja Bwana, katika ono, akanisahihisha. Naye akasema, ya kwamba, “Ushahidi wa Roho Mtakatifu ni wale ambao wangeweza kulipokea Neno”, wala si Upendo, wala kunena kwa Lunga, bali ni kulipokea Neno. (1Wathesalonike 1:4-6).

Halafu basi alikuwa akiniambia, ya kwamba, “Hilo ni maandiko,” maana katika Yohana 14, Yesu alisema, wakati yeye Roho Mtakatifu atakapowajilia atawafunulia mambo haya, ambayo nimewafundisha naye atawaonyesha mambo yajayo. (Yohana16:13). Kwa hiyo huo hapa Ushahidi halisi wa Roho Mtakatifu! Yeye hajaniambia bado jambo lolote ambalo si sahihi. Ya kwamba, Ushahidi wa Roho Mtakatifu, ni yeye anayeweza kuliadini Neno, kama unaweza kulipokea. “(Matendo 2:31, 1Wathesalonike 1:4-7). Maana, Yesu hakusema kamwe, Roho Mtakatifu akiisha kuja, mtanena kwa lunga.” Yeye hakusema kamwe, Roho Mtakatifu akiisha kuja mngefanya yoyote ya mambo haya. Lakini Yeye alisema, “Yeye atachukuwa mambo hayo yaliyo yangu na kuwapasha habari na mambo yajayo atawapasha habari zake.” Kwa hiyo hilo hapo Ushahidi halisi wa Roho Mtakatifu, kulingana na Yesu mwenyewe.

Swali la ndugu Branham: Nimebatizwa katika jina la Yesu. Neno lilisema mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Je hili linamaanisha Ubatizo, Roho Mtakatifu au lamaanisha yanipasa kupokea kile kipawa-dhahiri- yanipasa ni pokee, tukio dhahiri, kwa Ubatizo? Nina hamu ya kujazwa na Roho.

Sasa hilo ni swali zuri. Sasa ubatizo wa Roho Mtakatifu ni tukio dhahiri? Ambalo mtu lazima apokee. Sasa ninapoongea kuhusu kutokuamini kuwa Ishara madhubuti ya Roho Mtakatifu ni kunena kwa lugha (sikubaliani na hilo) naamini kwa msaada wa Mungu naweza kuthibitisha katika Biblia kuwa ni kipawa cha Roho Mtakatifu. Wangapi wanajua hilo? Uponyaji wa kiungu ni karama ya Roho Mtakatifu, na hapa Beatles wanafanya hivyo.

Sasa, hiyo si Ishara ya Roho Mtakatifu. Ona? Huwezi kuitegemea hiyo. Huwezi kutegemea tunda la Roho, kwa sababu tunda la kwanza la Roho ni Upendo. Na Christian science hufanya Upendo mwingi kuliko yeyote nimjuaye, na hata wao wanakana Yesu Kristo kuwa Mungu. Ona? Kuna Ishara moja pekee ya Roho Mtakatifu ninayojua, na hiyo ni Imani halisi katika Neno la wakati huo!

Kwa hiyo unaona? Makuhani hao walikuwa wapole, wanyenyekevu watu wenye akili. Ilipofikia matunda ya Roho, wangeonyesha matunda mengi zaidi ya Roho kuliko Yesu. Walikosa kuona Yeye alikuwa lile Neno lililoahidiwa la wakati ule. Njia pekee waliyokitambua Yesu alipotenda Neno kwa kuweza kuwaambia kile walichokuwa nacho moyoni mwao. Kile walichokuwa wakitenda... Yeye alikuwa Nabii kulingana na Neno la Mungu. Yale yeye alisema yalitimia, kila Neno, Neno kwa Neno.

Na, wao, walitambua, “oh! Musa, tuna Musa”. Yeye alisema “Kama mngalimjua Musa mngalinijua mimi, kwa kuwa yeye alinena habari zangu. “Bwana Mungu wenu atawaondokesha Nabii. Kama nilivyo mimi”. (kumbukumbu 18:15) Unaona sasa. Kwa hiyo Yesu alisema, kwenye Yohana 14, “wakati yeye, Roho Mtakatifu atakapokuja atawakumbusha mambo haya, awaonyeshe mnaishi katika siku gani na halafu jambo lingine litakalowafanya mjue yeye atawaonyesha mambo yajayo”. Unarudi moja kwa moja kwenye mambo ya unabii tena. “Atakapokuja”. Mnaona?

Kama nilivyo zungumzia juu ya garudumu lile ndani ya gurudumu, ama nafsi hiyo ya ndani kule ndani ya Roho. Jinsi ambavyo hiyo Roho ilivyo nje. Kati ya nafsi na mwili, inaweza kutiwa mafuta kabisa na Roho Mtakatifu. Nyote mlielewa na jambo hilo?

Sasa kufuatilia hilo pamoja na mwendeleo wa ujumbe, “Mungu wa ulimwengu huu”, watiwa mafuta katika siku za mwisho. Huo wa nje, mviringo huo katikati, mviringo wa kwanza ni hisia za mviringo wa pili ni hisia za Roho; hiari ya kibinafsi, shauku, na kadhalika. Bali wa ndani ni nafsi hiyo iliyochaguliwa tangu awali. Kwa hiyo wao wanaweza kuitia upako Roho hii, kuufanya mwili wa nje uwe chini ya utawala wa Roho. “Bali nafsi

itendayo dhambi, hiyo nafsi itakufa”. Nafsi inayokataa katika kutokuamini Neno la Mungu, ambalo ni sehemu yake, nafsi hiyo milele ita, imekuwa, daima.....

Ninaamini katika mauti ya milele, vile vile kama ninavyoamini katika Mbinguni ya milele, bali sio kuzimu ya milele. Hakuna kitu kama kuzimu ya milele. Kuna mauti ya milele kwa ajili ya watu ambao wengi wao walio wakidini katika ulimwengu leo, siku zote wamekuwa wafu.

“Mwanamke anayeishi katika anasa” na nywele zake zilizo katwa na uso wake uliopodolewa, “ni mfu angali anaishi”. Biblia ilisema hivyo mnaona? Mnaona, huenda akawa na dini, bali hakuwa ameokolewa kamwe, yeye anamsisimko wa nje. Huenda akaimba katika kwaya, ama huenda akacheza katika Roho, huenda akanena kwa Lugha na kuwa na udhihirisho wa Roho. Bali isipokuwa hiyo nafsi iliyo upande wa ndani ni binti wa Mungu, yeye amekwisha, haidhuru anafanya nini.

Angalia Neno hilo haliwezi kujikana lenyewe. Kwa hiyo ni shauku. Ni shauku ya nini? Ni nini kilikufanya uwe na shauku ya jambo hilo kwanza? Kwa maana huko ndani nafsini mwako kulikuwa na mbegu iliyo chaguliwa tangu awali ambayo ilikuwa uzima wa milele, daima imekaa humo ndani, daima ilikuwa humo ndani. “Wote alionipa Baba watakuja kwangu”. (Yohana 6:38) Hakuna hata mmoja wao atakayepotea”.

“Kondoo wangu huisikia sauti yangu, mgeni hawatamfuata”, kwa sababu mle ndani mna uzima, na uzima huungana na uzima. Dhambi huungana na dhambi, na dhambi ni nafiki sana hata inafikiri ya kwamba imeokolewa wakati haijakolewa. Iko kwenye kina cha ndani kabisa cha unafiki.

Vema, nini kinaivuta? Ni kitu fulani kule ndani kinachovuta. Nafsi inavuta nguvu zako kupitia nje kuingia rohoni, hata nafsini. Na kama hiyo nafsi inaipenda Dunia, imekufa. Sijali jinsi ilivyotiwa mafuta, ni huku nje, na jinsi ilivyo yenye haki huku nje; humu chini imekufa kwa kuwa yeye aipendaye dunia au mambo ya dunia, kumpenda Mungu hata hakumo ndani yake, haidhuru ni mtu wa dini namna gani. (1Yohana 2:15-17).

Chujio la kweli, kwa jinsi hiyo, litaweka mambo hayo yote nje na yasilete kitu chochote ila ukweli wa Mungu, Neno katika ile nafsi iliyo halisi na ya kweli.

Sasa ukitaka dhihirisho la Roho Mtakatifu, hilo hapo, wakati nafsi hiyo yako itakapoungana na Neno la Mungu, katika kila hali, inaonyesha umeyavuta maisha yako kupitia katika chujio la Mungu.

Halafu hilo linaonyesha ya kwamba ndani yako kulikuwemo na uzao uliochaguliwa tangu awali ndani yako, ambao unakufanya umuonee Mungu njaa. “Wote alionipa Baba yangu alionipa kuwakomboa; walikufa pamoja nami pale kalvari; walifufuka pamoja nami katika ule ufufuo; wote alionipa mimi, watakuja kwangu watawekwa katika mwili, ambapo mguu, mkono, pua, mdomo, hata iwe nini; vitawekwa mle ndani. Nao watakuja kwangu katika majira yao.

Kama ile mbegu iliyochaguliwa tangu awali haimo mle, halitavutiwa mle, kwa maana inavuta kwa ajili ya shauku yake.

Na kitu pekee unachoweza kuvutia katika Neno la Mungu ni Roho, ile nguvu ya kuhuisha kulifanya Neno lenyewe, ambalo limo ndani yako, liishi likamdhihirishe Yesu Kristo katika wakati huo unaoishi. Haleluya! Ndugu, kama hiyo si kweli, sijui kweli ni nini, mimi nimerukwa na akili iwapo hiyo si kweli.

Ni Neno lenyewe moyoni mwako, lililokusudiwa humo tangu awali ambalo linavuta. Nalo linautema huo Ulimwengu; haliutaki. Bali wakati linapofika hapa kwenye Neno, haliwezi kuwa kitu kingine ila Roho Mtakatifu kulihuisha Neno hilo.

Kwa hivyo kuwa mwanatheologia aliyefuzu sana halihusiani nalo. Kuwa mnyenyekevu na mpole halihusiani nalo. Nini kilimfanya Yeye tofauti? Yeye Yesu alikuwa Neno lilifanyika mwili, (Yohana 1:1-3,14), si lile Neno la siku za Musa, Musa alikuwa siku hiyo, Neno; si lile Neno la siku za Nuhu, Nuhu alikuwa Neno kwa siku hiyo; si siku ile-Neno lile la siku za Eliya, Eliya alikuwa Neno la siku hiyo; lakini Yeye alikuwa Neno la wakati uliopo, nao walikuwa wakiishi katika yaliyopita.

Jambo lile lile lajirudia! Hiyo Ishara ya Roho Mtakatifu, Mungu alipofunuliwa na unaliona, Bwana asema hivi na kulikubali. Si vile ulivyo, vile ulivyokuwa, au lolote lile, ni yale Mungu amekufanyia wewe sasa. Hiyo ndiyo Ishara.

Yesu alisema..... Yeye alitupa Ishara ya Roho Mtakatifu, Yohana 14, Yeye alisema, Ninayo mengi ya kuwaambia, sina wakati wa kuwaambia, lakini Roho Mtakatifu atakapokuja, Yeye atawaambi, atawakumbusha yote niliyo waambia, na mambo yajayo atawapasha habari zake. Hamuoni? Hiyo ndiyo Ishara. Huko ni kutabiri na kuwa na tafsiri ya kiungu ya Neno lililoandikwa. Sasa, si hiyo ndiyo Ishara ya Nabii?

Mwonaji katika Biblia alikuwa mtu ambaye angetabiri na ingetimilika, kabisa, si eti mtu fulani alimwekea mikono, hicho ni kipawa. Nabii anachaguliwa tangu awali na kuzaliwa nabii. Unaona? Maisha yote alikuwa Nabii; hiyo ni huduma. Hapo ndipo watu.....

Mengi ya maswali haya hapo juu ya: “Vema, je, Bibi Arusi ata... je, hili lita? Kanisa na ...ona? Hu-huwezi kutenganisha yalivyo. Bibi Arusi ni Mteule wa Mungu. Kanisa litapita..... Hao ndio wale hilo linasema, “Yeye atakaye na aje”. Lakini Bibi Arusi ni mteule wa Mungu. (Ufunuo 22:17) (1 Wakorintho 13:10) yasema haya. “Ijapo ile iliyo kamili, iliyo kwa sehemu itabatilika”. Kwa hiyo mambo haya yote madogo madogo ya kuruka juu na chini kama mtoto, kujaribu kunena kwa lugha, na mambo haya yote, ijapo ile iliyokamili... **Nasi tunayo siku hizi, kwa msaada wa Mungu, ile tafsiri kamilifu ya Neno na thibitisho la kiungu!** Basi ile iliyo kwa sehemu imebatilishwa. Nilipokuwa mtoto mchanga, nilisema kama mtoto mchanga, nilifahamu kama mtoto mchanga; tokea hapo nilipokuwa mtu mzima, nimeyabatilisha mambo ya kitoto” Amina!

Hapa palikuwepo na jibu pia la Mt.7:21-23. Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana atakayeingia katika Ufalme wa Mbinguni, bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni. Wengi wataniambia siku ile, Bwana Bwana hatukufanya Unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo na kwa jina lako kufanya miujiza mingi? Ndipo nitawaambia dhahiri, sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu. **Yesu hakatai ya kwamba wao walifanya kazi kuu ambazo Roho Mtakatifu ndiye tu anayeweza kutimiza kwa njia ya wanadamu. Lakini yeye alikana kwamba hajawahi kuwajua. Hawakuwa waliorudi nyuma walikuwa watu waovu, wasioongoka, wakana Imani. Hawa walikuwa mbegu ya shetani.**

Na ndilo hilo hapo. Huwezi kudai ya kwamba dhihirisho ndio ushuhuda wa kuzaliwa na Roho. Kujazwa na Roho. La bwana. Nitakubali ya kwamba dhihirisho la kweli ni ushuhuda wa Roho Mtakatifu akifanya kazi kuu. Lakini si thibitisho la yule mtu binafsi kujazwa na Roho, hata ingawa mtu huyo binafsi ana wingi wa madhihirisho hayo.

Ushuhuda wa kumpokea Roho Mtakatifu leo ni kama vile vile tu ilivyokuwa katika siku za Bwana wetu. Ni kulipokea Neno la kweli kwa siku ile unayoishi. Yesu kamwe hakutilia mkazo umuhimu wa kazi kama alivyotilia maanani sana Neno. Alijua ya kwamba kama watu wakilipata Neno kazi zingefuata nyuma. Hiyo ni Biblia. Sasa Yesu alijua ya kwamba kutakuweko na kutoka kwenye Neno kubaya sana katika wakati wa Pergamo ambao

ulikuwa bado umbali wa miaka mia mbili kutoka kwenye lile ono la patmo. Alijua ya kwamba kutoka huko kungewafanya kuingia katika zile zama za Giza. Alijua ya kwamba jinsi mwanadamu hapo awali alivyotoka kwa Mungu ilikua kwanza kwa kuliacha Neno. Kama ukiliacha hilo Neno, Umemuacha Mungu.

Hivyo basi anajitambulisha mwenyewe kwa Kanisa hapo Pergamo na kwa kweli kwa makanisa yote ya nyakati zote “Mimi ni Neno”. Kama mkitaka Uungu kati yenu, basi karibisheni na mlipokee Neno. Msiache mtu yeyote hata wala chochote kiingie kati yenu na hilo Neno. Hiki ninachowapa ninyi (Neno) ni ufunuo wangu mwenyewe. Mimi ni NENO kumbukeni hilo.

Ushuhuda ni udhihirisho wa Neno katika saa unayoishi. Walikuwa na Biblia. Ilikuwa halisi tu kile Yehova alisema kingelitokea. Halihitaji tafsiri yoyote. Ilitafsiriwa hapa. Kulikuwa na Makuhani wako, kulikuwa na yote waliyokuwa nayo, na kila kitu kingine kilikuwa kwenye utaratibu tu, na kila kitu, lakini bado walishindwa kuliona Neno. Na alilifanya Neno hilo liishi kwa wakati huo, hiyo ndiyo ushuhuda wa wakati huo.

Lutha alikuwa na ushuhuda wa wakati wake, Wesley wa wakati wake, Pentekoste wa wakati wake, lakini tuko katika mwingine. Mambo haya ni mazuri, lakini kama mtoto, ana kidole, jicho na pua, bali baada ya kitambo kidogo anakuwa mwanadamu. Hana budi kuwa mtoto aliyekomaa kasha azaliwe ana nafsi, mwili, roho, anaweza kutembea tembea.

Na tunagundua ya kwamba, yote haya, Yesu ametangaza. Na katika uchache tu, hao tu ambao amewasaidia uzima, waliomuona, sio kundi kubwa; halingeweza kuwa kubwa kama la Kayafa kwa nini, angeliweza kuliita Taifa zima pamoja. Yesu aliita wachache tu pamoja. Sio wengi walio mtambua. Elfu mara elfu, wakati alipokuja ulimwenguni. Alipita ulimwenguni na kamwe hata hawakujua alikuwa hapa.

Na siku zote kumekuwa safina katika uchumi wa Mungu. Ili kuwepo safina katika siku za Nuhu. Kwa kuwaokolea watu wake. Kulikuwepo na safina katika siku za sheria, safina (Sanduku) la shuhuda katika siku za sheria, Walilifuata sanduku, na sasa kuna wakati watatu wa badiliko, sasa, kama wakati wa Nuhu wakati wa Lutu, na sasa wakati huu. Kuna safina sasa, na safina hiyo sio dhehebu; na wala si kazi njema ambazo unazifanya; ni kwa Roho mmoja. (Warumi 8:1). Sisi sote tulibatizwa katika mwili mmoja katika mamlaka ya ule ufalme, ubatizo mmoja wa kiroho. Haijalishi jinsi gani ulivyo mwema, jinsi ulivyo mbaya. Vyovyote uko katika Ufalme huo kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Unaona? Hiyo ndiyo njia pekee utakayo shinda.

Ni wote ambao wako chini ya damu iliyomwagika ndio washindi, sababu huwezi kushinda mwenyewe; ni yeye ambaye anakushindia. Umepumzika. Nitajuaje tena, Ndugu Branham, kwamba niko hapo? Angalia ni maisha ya jinsi gani unayoishi. Tazama tu. Ona kama unajiishia tu bila kujilazimisha. Au je unajilazimisha na kujisukuma, hapo ujue unatenda wewe, usijaribu kulifanya mwenyewe.

Thibitisho la Roho Mtakatifu ni wakati unapoweza kulipokea Neno; si taratibu fulani, bali kupata kuelewa vizuri. Unajuaje ya kwamba Neno ni wazi, unalifahamu hilo? Liangalie likijithibitisha lenyewe. “Vema” manasema “Ninaona hili likifanya kitu hiki, na kile”. loo! Naam, magugu yanaishi kwa njia ileile. Bali haina budi kuwa ni Neno lote. Kuwa Bibi Arusi huna budi kuwa sehemu yake. Yeye ni Neno mnaona? Na ni sehemu gani ya Yeye? Neno lililoahidiwa kwa ajili ya siku hii wakati Yeye amwitapo Bibi Arusi wake. Ninyi ni sehemu ya hilo. Mnalipata? Sasa, msiachilie hilo sasa.

Waliochaguliwa tangu zamani ndio tu wafanyao jambo hilo; ndio tu wanaoweza. Nawe waweza kulifanya sababu, angalia, inathibitisha uteule maana kama una uzima wa milele, ilikubudi uwe sehemu ya Mungu wakati wote, maana yeye ndiye tu wa milele. Mnaona jambo hilo? Loo, jamani wazia jombo hilo. Sasa angalia jambo linalotukia katika ule utawala mkuu wa miaka elfu. Jambo pekee, mkombozi amekufanya wewe utambue jambo hilo. Nawe daima ulikuwa hivyo, na ndio sababu unaona siku unayoishi. Siku tunayoishi, unaitambua... Sasa, Mmethodisti alisema, “Unapopiga makelele, umempata huyo”. Wengi walipiga makelele, wala hawakumpata huyo, Mpendekoste alisema, “ Wakati unaponena kwa lugha, unaye huyo”. Wengi walinena kwa lugha wala hawakuwa naye. Angalia jinsi, kila namna ya taratibu walizokuwa nazo mafarisayo wale, bali wakati Neno linapodhihirishwa, wao hawakulitambua hilo.

Serikali inapotia muhuri juu ya furushi, idara ya reli ikitia muhuri mlangoni, behewa hilo haliwezi kuguswa hata litakapofika mwisho wa safari yake. Mungu anapoutia muhuri wake juu ya mtu fulani. (Na muhuri huo ni Roho Mtakatifu). Anapomtia muhuri mtu namna hiyo, yeye tayari ameenda kwenye kikomo cha milele. Naye hawezi kamwe, kamwe kurudi nyuma tena. Maana kumbukeni, (Waefeso 4:30) Inasema msimhuzunishe yule Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwa yeye mlitiwa muhuri daima. Mnaona? Mmetiwa muhuri milele. Mmetiwa muhuri, milele katika Ufalme wa Mungu, kwa Roho Mtakatifu. Sasa wazieni jambo hilo! Basi, wewe Ibilisi atakutupia ngumi, na atakuambia kila kitu, na kukushtaki, na-na kukujaribu kukufanya wewe ufikiri ya kwamba wewe siye. Bali usimsikilize. Sasa unajua umepita mautini kuingia uzimani. Unajua mambo ambayo wakati mmoja uliyatenda,

huyapendi tena. Unajua ya kwamba umeamini kila Neno la Mungu, umemuona Mungu akifanya kazi papa hapa miongoni mwetu.

Kimsingi una ile arabuni, kwa kungoja (2Korintho 1:20-2). Sasa, unapopata zile nguvu za utendaji, umehuishwa kutoka anayepatikana na mauti ukiwa asiyepatikana na mauti (Waefeso 2:1-7), inaufanya mwili wote ulitii Neno. Litakufanya utende tofauti, uonekane tofauti uishi tofauti. Hilo litakufanya tofauti tu. Sasa, wawezaje kudai ya kwamba una Roho, halafu ujitupe mbali na Neno? Umehuishwa na kitu kingine. Kwa kuwa, Huyo ataihuisha kwenye Neno miili yenu iliyo katika hali ya kufa (Warumi 8:11). Hakika ataihuisha atawafanya mfanye mambo ambayo hakufanya hapo awali. Wao walikuwa wamejaa nguvu za kuhuisha wakati huo. Mnaona? Mwili wako hauko chini ya dhambi tena; angalia ni kama tu mbegu ndogo iliyo ardhini. Sasa, namna ya kiroho umefufuka unapompokea Roho Mtakatifu ndani yako. Umefufuka. Umefufuka papo hapo. (Warumi 6:1-2). Mwili wako kwa uwezekano umefufuka. Angalia, njiani, unapoendelea kukuwa kufikia ukamilifu wa ufufuo, ukiongozwa na Roho (Warumi 8:14-43). Sasa angalia wawezaje kusema ya kwamba Roho huyo anaishi ndani yako ingawa ulifanya kila kitu ulichofikiria kilikuwa sawa? Huu hapa ushuhuda wako kama unaye huyo ama huna. Ikiwa Roho aliye katika Kristo ana kaa ndani yako, Yeye pia anakuhuisha kwenye Neno, basi huyo si Roho wa Kristo. Sijali unayofanya, mpaka huyo atakapokupeleka kwenye Neno. “Kondoo zangu wanaisikia sauti yangu nao waishi kwa kila Neno”. Kila Neno!.

Basi uzima ule uliokuwa katika Kristo ni Roho Mtakatifu, si nafsi ya tatu, lakini nafsi ile ile, katika mfano wa Roho Mtakatifu, akija juu yako, kama Ishara ya kwamba uzima wako na nauli yako vimelipiwa, umekubalika mpaka Ishara hiyo itakapokuja huruhusiwi kwenye barabara kuu, (Isaya 35:8-10) huruhusiwi kwenye shirika la mabasi, huruhusiwi kuingia mpaka uweze kuonyesha Ishara hii, na Ishara hiyo ndiyo nauli yako. Na sasa hiyo inaonyesha ya kwamba ile damu imekwisha kumwagika na imepakwa kwako, gharama imelipwa, nawe unaishara ya kwamba umepakwa ile damu na umekubalika. Mmeelewa sasa? Loo, jamani loo! Sasa si thibitisho fulani tu unaona? Unasema, “Ndugu Branham”, (ninalihisi moyoni mwenu mnaona) nitajuaje? Angalia ulichokuwa na ulicho sasa? Hivyo ndivyo unavyojua. Unaona sasa? Hivyo ndivyo unavyojua. Unaona? Ulikuwa nini kabla Ishara hii haijawekwa? Wewe ni nini baada ya hiyo kuwekwa? Shauku yako ilikuwa ni nini hapo kabla na shauku zako ni nini baadaye? Ndipo unajua kama ile ishara imewekwa ama haijawekwa. Na mambo haya mengine yanaambatana tu na hiyo moja kwa moja.

Ni kama kuzungumza juu ya hilo, na kusema “Lugha ndio ushahidi” sasa, nilinunua jozi ya viatu usemi wa kiatu sicho kiatu hicho kinakuja tu na kiatu

hicho, unaona huja tu na kiatu. Unaona? Basi na Ishara ni vile vile. Ile Ishara ni Kristo. Lakini kunena kwa Lugha, na kutoa pepo na kufanya mambo hayo yote na kuhubiri na chochote kile ni ushahidi ya kwamba ipo, kweli lakini sio hivyo, mnaona? Ni kipawa chake. Kama nitakuambi kwamba... unasema, ninakutakia wewe Ndugu Branham; na mimi nitoe zawadi nikupe, vema, hiyo si mimi, hiyo ni zawadi yangu. Lugha ni kipawa cha Roho Mtakatifu si Roho Mtakatifu; kipawa cha Roho Mtakatifu. Na ibilisi anaweza kuiga chochote cha mambo hayo, lakini hawezi kuwa Roho Mtakatifu unaona? Anaweza kuigiza hizi karama lakini hawezi kuwa Roho Mtakatifu. Na Roho Mtakatifu ni Ishara ya kwamba ile damu imepakwa, kwa maana yeye anafuata damu siku zote katika kitabu cha ukombozi.

Swali: Nini Ishara madhubuti kuwa mtu hakika amejazwa Roho Mtakatifu? (Yohana 14:26) “Lakini huyo Roho Mtakatifu ajapo atawaonyesha mambo yote yajayo” Ona! Yeye atayakamilisha; “Yaliyo tengenezwa na mwanadamu” hayatafaa kitu; na Yeye ni Neno. Huyo Roho Mtakatifu ajapo yeye atajitambulisha mwenyewe ndani yako kwa maandiko. Na hiyo ndiyo Ishara halisi kuwa Roho Mtakatifu yumo ndani yako kwa sababu yeye ni Neno.

Nukuu

Mabirika yavujayo para 66-68.

Maswali na majibu mwaka 64-08-23 jioni Uk1001,SW,No281/uk 1004, par48-53,57/uk 1040,sw.No 318.

Makao ya baadaye-para 270-269,195-197,260-266.

Chujio la mtu mwenye busara para67-70,104-109,114-115,122,133,138-139.

Wakati wa kanisa la Pergamo Uk 169.

Kisha Yesu akaja na kuita para 22-25 (64-02-13).

Jinsi gani nitaweza kushinda para 68-73.

Je Mungu hubadilisha nia yake para 4-7.

Ni kuchomoza kwa jua Uk 28,29,31.

Kukata tamaa para 17-20.

jiwe la kiroho la kujengea na 131 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, iliyokusanywa na Gerd Rodewald Friedenstr. 69 D – 75328 Schomberg, Germany (+49) 72357613 Fax : (+49) 72353306. www.biblebelievers.de

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itaizunguka dunia na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia. (Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)

Kwa nakala zaidi: kiingereza, kiswahili, andika kwa:

Charles E. Y. Kanju,

Box 553 Korogwe - Tanga

E-mail: Chaelika@live1.com

Cellphone: 0784 704299/ 0718230098